# haki zako na ulinzi dhidi ya salio la malipo na bili za matibabu za ghafla

**Unapopata huduma ya dharura au kutibiwa na mtoa huduma wa nje ya mpango wako katika hospitali iliyoko ndani ya mpango wako au kituo cha upasuaji cha bila kulazwa, umelindwa dhidi ya kulipa bili ya ghafla au bili ya salio.**

- Ulinzi huu **HUWAHUSU** wagonjwa walio chini ya mipango ya afya ya vikundi na watu binafsi kama vile washiriki wa bima ya afya ya kibinafsi.
- Ulinzi huu **HAUMHUSU** mtu yeyote mwenye bima ya Medicare, Medicaid, Indian Health Services, Veterans Affairs Health Care, au TRICARE kwa kuwa mipango hii tayari ina ulinzi wa ndani wa malipo.

## Je, bili ya salio ni nini *(wakati mwingine huitwa "bili za ghafla")*?

Unapomwona daktari au mhudumu mwingine wa afya, unaweza kudaiwa gharama fulani unayolipia kwa kutumia pesa zako, kama vile kiasi unacholipa wakati wa huduma(copayment), asilimia unayolipa baada ya makato (coinsurance) na/au makato. Unaweza kuwa na gharama nyingine au kulipa bili nzima ukimwona mtoa huduma au kutembelea kituo cha afya kisicho kwenye mpango wako wa afya.

"Nje ya mpango" inamaanisha watoa huduma na hospitali ambazo hazijatia saini mkataba na mpango wako wa afya. Watoa huduma walio nje ya mpango wako wanaweza kuruhusiwa kukutoza tofauti kati ya pesa ambazo mpango wako ulikubali kulipa na bili nzima inayodaiwa kwa ajili ya huduma. Hii inajulikana kama "**bili ya salio.**" Kiasi hiki kinaweza kuwa zaidi ya gharama ya watoa huduma walioko kwenye mpango wako kwa huduma sawa na huenda kisihesabiwe kwenye kiasi cha pesa unazolipa kila mwaka kutoka mfukoni mwako.

"**Bili ya ghafla**" ni bili ya gharama isiyotarajiwa. Hili linaweza kutokea wakati huwezi kudhibiti ni nani anahusika katika utunzaji wako — kama vile wakati una dharura au unaporatibu ziara katika kituo kilicho kwenye mpango wako lakini unatibiwa bila kutarajia na mtoa huduma wa nje ya mpango wako.

## umelindwa dhidi ya kulipa bili ya salio kwa:

**Huduma za dharura**

Ikiwa una hali ya dharura ya matibabu na kupata huduma za dharura kutoka kwa mtoa huduma au kituo kisicho kwenye mpango wako, kiasi kikubwa ambacho mtoa huduma au kituo hicho kinaweza kukutoza ni kiasi cha mpango wako cha kugawana gharama ndani ya mpango wako (kama vile copayments na coinsurance). Huwezi kulipishwa salio la bili kwa huduma za dharura. Hii ni pamoja na huduma unazoweza kupata baada ya hali yako kuwa dhabiti *isipokuwa* ukitoa idhini iliyoandikwa na kukubali kulipishwa bili ya salio kwa huduma hizi za baada ya kuwa dhabiti.

**Huduma fulani kwenye hospitali iliyoko kwenye mpango wako au kituo cha upasuaji cha bila kulazwa**

Unapopata huduma kwenye hospitali iliyoko kwenye mpango wako au kituo cha upasuaji cha bila kulazwa, watoa huduma fulani hapo wanaweza wasiwe kwenye mpango wako. Katika hali kama hizi, kiasi kikubwa ambacho watoa huduma hao wanaweza kukutoza ni kiasi cha kugawana gharama cha mpango wako. Hii inatumika kwa dawa ya dharura, nusukaputi, patholojia, radiolojia, maabara, neonatolojia, usaidizi wa hospitali na huduma za wagonjwa mahututi. Watoa huduma hawa hawawezi kukutoza na hawapaswi kukuambia utoe idhini ya kulipishwa salio la bili.

Ukipata huduma zingine katika vituo vilivyo kwenye mpango wako, watoa huduma wa nje ya mpango wako hawawezi kukulipisha bili ya salio isipokuwa utoe idhini ya maandishi na kukubali kulipa.

dayton children's

**Huhitajiki kamwe kukubali kuli pishwa bili ya salio. Pia huhitajiki kupata huduma kwa wahudumu wasio kwenye m pango wako. Unaweza kuchagua mtoa huduma au kituo kilicho kwenye m pango wako.**

## wakati malipo ya salio la bili hayaruhusiwi, pia una haki zifuatazo:

1. Una wajibu wa kulipa sehemu yako ya gharama tu (kama vile copayments, coinsurance, na makato ambayo ungelipa ikiwa mtoa huduma au kituo kingekuwa ndani ya mpango wako). Mpango wako wa afya utalipa watoa huduma na vituo visivyo kwenye mpango wako moja kwa moja.

2. Mpango wako wa afya kwa jumla lazima:

    a. Ugharamie huduma za dharura bila kukuhitaji upate idhini ya huduma mapema ("idhini ya awali").

    b. Ugharamie huduma za dharura kutoka kwa watoa huduma wasio kwenye mpango wako.

    c. Uhesabu kiasi unachodaiwa na mtoa huduma au kituo ("gharama ya kugawana") kulingana na kiasi ambacho kitamplipa mtoa huduma au kituo kilicho ndani ya mpango wako kisha uonyeshe kiasi hicho katika maelezo yako ya manufaa.

    d. Hesabu kiasi chochote unacholipa kwa huduma za dharura au huduma za nje ya mpango wako na kujumuisha kwenye kiasi chako makato na kiasi cha pesa unazotoa mfukoni.

## ikiwa unaamini kwamba umetozwa kimakosa:

Ikiwa unaamini kwamba umetozwa kimakosa, unaweza kuwasiliana na kituo cha U.S. Centers for Medicare & Medicaid Services (“CMS”) kupitia 1-800-985-3059 au cms.gov/nosurprises. Unaweza pia kuwasiliana na Ohio Department of Insurance (“ODI”) kupitia 1-614-644-2658 au insurance. ohio.gov/strategic -initiatives/ surprise-billing/ resources. Tovuti zote mbili zina maelezo ya ziada kuhusu ulinzi dhidi ya salio la malipo na bili ya ghafla.

## Bei na makadirio ya gharama ya Hospitali ya Watoto ya Dayton

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu gharama ya utaratibu au huduma yoyote ya Hospitali ya Watoto ya Dayton, tafadhali nenda kwenye zana ya hospitali ya mtandaoni ya bei na kukadiria gharama: childrensdayton.org/ pricing-cost-estimation

dayton children's
above and beyond

EP11938 © 2022 Hospitali ya Watoto ya Dayton Haki Zote Zimehifadhiwa. Whirligig, Ishara ya Nembo na chapa zote za biashara zinamilikiwa na Hospitali ya Watoto ya Dayton • childrensdayton.org